Kikao cha Sita – Tarehe 10 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 11:00 jioni)

Dua

Mhe.Naibu Spika, (Mhe. Ali Abdalla Ali) Alisoma Dua

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.

19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura

46.Mhe. Hassan Hamad Omar Jimbo la Kojani

47.Mhe. Hija Hassan Hija Jimbo la Kiwani

48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Jimbo la Bububu

49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu Jimbo la Mji Mkongwe

50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub Jimbo la Muyuni

51.Mhe. Kazija Khamis Kona Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid Jimbo la Kiembesamaki

55.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahakama Kuu) ya mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, jana tuliwamalizia wachangiaji wote, kwa hivyo leo tutafanya majumuisho. Kwanza tutamkaribisha Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ili afanye majumuisho na baadae tupitishe vifungu. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kurudi hapa tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Naibu Spika, mswada ambao upo mbele yetu ni Mswada wa Kuanzisha Mahakama ya Biashara. Katika mswada huu kuna wachangiaji karibu 16 na napenda niwashukuru sana wachangiaji hawa ambao kwa kweli mawazo yao na maelekezo yao ni mazuri na tutayazingatia zaidi katika kuufanya mswada huu kuwa mzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda niishukuru Kamati ya Katiba na Sheria, kwa sababu Kamati hii ndio ya mwanzo iliyotoa maelekezo pamoja na masahihisho mengi ambayo walitupa, kwa bahati nzuri kama nilivyosema juzi ni kwamba masahihisho hayo yote tuliyaweka.

Pili, napenda niwashukuru Wajumbe wote wale waliochangia kwa michango yao mizuri ambayo imetusaidia. Kwa nafasi hii naomba niwataje wachangiaji wenyewe ambao ni 16:

1. Mhe. Panya Ali Abdalla Mhe.
2. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ussi Jecha Simai
4. Mhe. Mohamed Haji Khalid
5. Mhe. Subeit Khamis Faki
6. Mhe. Salmin Awadh Salmin
7. Mhe. Asha Bakari Makame
8. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
9. Mhe. Hassan Hamad Omar
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
12. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
13. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
14. Mhe. Hija Hassan Hija
15. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

16. Mhe. Mussa Ali Hassan

Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wote hawa walichangia katika maeneo muhimu, na kwa bahati nzuri nilivi-*note* vile vifungu vyote ambavyo walivitaja wakati wa kuchangia. Wote hawa walichangia katika vifungu 20. Kifungu cha 1, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 11, 13, 14, 16, 17, 18, 24, 30, 31, 33, 36, 39, na kifungu cha 40. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wachangiaji wote hawa walichangia katika vifungu vya aina moja. Kwa hivyo, naomba nitoe majumuisho haya kwa pamoja, ili wote wale waliochangia watajua kwamba jibu lao nimeshalitaja.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 1 kilikuwa kinazungumzia tarehe ya kutumika kwa mswada ule. Mhe. Subeit alisema kwa nini Waziri ataitangaza, je Rais ni lazima awe ametia saini. Napenda niseme tu kwa ufafanuzi zaidi wa Baraza ni kwamba mswada hauwi sheria mpaka kwanza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Rais wote waukubali. Kwa hivyo, hicho ni kitendo cha mwanzo kwamba lazima saini ya Mhe. Rais ipatikane ndio mswada uweze kuwa sheria. Lakini sheria zipo nyengine ambazo zinataja tarehe ya kuanza, lakini hata kama itataja tarehe ya kuanza lakini ni lazima Rais atie saini, ili iwe ni sheria.

Kwa mfano, hata ukitizama Katiba katika kifungu cha mwisho kule kinasema kwamba katiba hii itaanza kutumika tarehe 12 Januari 1985. Ukitizama kwa mfano sheria ya usafiri wa baharini *Maritime Transport Act*, imeelezea wazi katika kifungu cha mwanzo kwamba sheria hii itaanza kutumika pale ambapo Waziri atatangaza kwenye gazeti. Kwa hivyo, huu ni utaratibu wa kikawaida tu. Mara nyengine inakuwa hivyo, kwa sababu hata ukipitisha sheria kuna baadhi ya mambo ni lazima yakamilike ili ile sheria ianze.

Kwa mfano, kuna kanuni zinataka kufanywa au kuna utaratibu mwengine unataka kuchukuliwa. Kwa hivyo, likitokea kama hili ndio ile sheria inasema kwamba sheria hii itaanza kutumika tarehe kadhaa, au itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza. Kwa hivyo, hiki sio kitu cha kushtukia tu ni uandishi wa kawaida katika sheria zetu.

Kifungu cha 3, 4 na cha 5 Mhe. Naibu Spika, kilizungumziwa sana kuhusu nini maana hasa ya biashara au kesi hizi za biashara. Mhe. Naibu Spika, ukisoma katika kifungu cha 3 kwenye tafsiri, inasema kwamba

Kifungu cha 3

> “Kesi ya biashara maana yake ni kesi ya madai inayohusisha jambo linachukuliwa na mahakama kuwa ni la kibiashara, likijumuisha lalamiko lolote au ombi lolote litokanalo na tendo la kibiashara. Lakini halifungiki na mambo yale ambayo yamewekwa pale”.

Lakini pia ukisoma kifungu cha 5 kinasema kwamba;

Kifungu cha 5

> “Mahakama ya Biashara itakuwa na mamlaka inayofuata”

Pale imetaja mambo Mahakama ya Biashara itahusika. Lakini katika kifungu cha 5(3) pia imeweka Mamlaka ya Mahakama ya Biashara ambayo imewekwa ile idadi yake ya fedha ambazo mahakama ile inaweza ikatumia.

Kwa mfano, wamesema kwamba Mamlaka ya Mahakama ya Biashara yataweza kutumia kwa malalamiko ya kibiashara ambayo yanazidi shilingi milioni 30, pale ambapo jambo linalobishaniwa ni mali inayoondosheka na mali isiyokamatika inayozidi shilingi milioni 20 na inayowezekana kutathminiwa katika kiwango cha fedha na isiyopungua shilingi milioni 50. Kwa hivyo, kesi zote zenye kima hiki, hizo zitakwenda kwenye mahakama ya biashara. Kwa hivyo, ukisoma kifungu cha 3 na ukisoma kifungu cha 5, ina maana kwamba kuna kesi nyengine ambazo zimetolewa katika mamlaka ya kesi ya mahakama ya kibiashara.

Kwa mfano, kuna Mwakilishi mmoja hapa alizungumza na akasema kwamba kila kitu ni biashara. Ni kweli, ukienda Darajani wauza mitumba wale ni biashara, nguo zile ni biashara. Lakini kesi kama zile ndogo ndogo hazihusiani kabisa na mahakama hii. Lengo la mahakama hii Mhe. Naibu Spika, ni kuwafanya wale wenye biashara kubwa. Kwa mfano, wenye mahoteli na wenye miradi mikubwa mikubwa, wale inapotokezea tatizo, wanapokwenda katika mahakama za kawaida inachukua muda mrefu sana, na kwa sababu hiyo ndio ikatungwa sheria hii ili kupunguzwa ule muda ambao unaweza kuchukuliwa katika mahakama zile.

Kwa hivyo, hii Mhe. Naibu Spika, napenda niseme tu na Wajumbe wafahamu kwamba haitoingiza zile biashara ndogo ndogo kama zilizotajwa jana na juzi kuwa zinaingia katika mamlaka ya mahakama hii ya biashara. Mahakama ya biashara hii itahusiana na kesi tu zile ambazo kima chake kimewekwa katika kifungu cha 5(3).

Mhe. Naibu Spika, pia ilizungumziwa kuhusu ile idadi au *composition* ya mahakama. Katika kifungu cha 6 tulisema kwamba mahakama itajumuisha Jaji atakayeteuliwa na Jaji Mkuu miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu na washauri wawili miongoni mwa watu walioteuliwa na kamati ya watumiaji wa mahakama ya biashara iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 7. Sasa ile mahakama ya biashara inapokaa kusikiliza kesi itakuwa na watu 3. Jaji ambaye aliteuliwa pamoja na washauri wawili. Lakini hao washauri wawili hawatoki popote tu, kuna kamati ya watumiaji wa mahakama ya biashara ambayo hiyo ndio itakayopendekeza watu wawili, ili wachanganyike na Jaji, na Jaji huyo tena ile itakuwa ndio *composition* ya mahakama ya biashara.

Katika kifungu cha 7 na cha 9 Mhe. Naibu Spika, lilizungumzwa kwamba mahakama inapomuita mtu yeyote kuwa rafiki yake, inazingatia uwezo wa mtu. Maana yake ilizungumzwa hapa. Pale tunasema kwamba mahakama itaita mtu yeyote kuwa ni rafiki wa mahakama. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, mahakama ina uwezo wa kumuita mtu yeyote kwamba ni rafiki wa mahakama. Madhumuni hasa ya kumuita mtu kama ni rafiki wa mahakama ni kwamba kuna kesi mbele ya mahakama, au kuna shauri mbele ya mahakama.

Sasa ili kupata utatuzi au kupata ufafanuzi zaidi wa mambo, basi mtu fulani anao ujuzi huo. Kwa hivyo, kutokana na ujuzi wake au kutokana na uzoefu wake basi mahakama inaweza kumuita mtu yule kama ni rafiki wa mahakama ili aeleze uzoefu wake katika suala lile, aeleze ujuzi wake katika suala lile na aeleze kwa ujumla katika suala lile liliopo mbele ya mahakama yeye analifikiria vipi. Kwa hivyo, mahakama inapofanya hivyo, ndio inakuwa mahakama inamuita mtu, na mtu yule anaitwa ni rafiki wa mahakama.

Kwa hivyo, hapa Mhe. Naibu Spika, napenda niwahakikishie Wajumbe kwamba mahakama haiiti tu mtu yeyote inayemtaka, hapana. Ni lazima kuna utaratibu maalum ambao unafuatwa ili mtu yule aitwe kutoa ushauri wake.

Nakumbuka Mhe. Naibu Spika, sina uhakika ni wa kesi gani, lakini hata na Mwanasheria Mkuu wetu aliitwa zamani kidogo katika mahakama ya rufaa ya Bara kama yeye ni rafiki wa Mahakama. Sasa inapotokea kama hivyo, ndio rafiki wa mahakama anavyofanywa na anavyoitwa.

Suala jengine ambalo liliulizwa katika kifungu cha 8, inazungumza kwamba kutakuwa na wafanyakazi wa mahakama ambao watakuwa ni maafisa katika utumishi wa mahakama. Wakauliza je wafanyakazi hawa watakuwa ni sawa sawa na wafanyakazi wa mahakama za kawaida. Jibu ni ndio, kwa sababu hii tulisema na hata ukitizama katika kifungu cha mwanzo, tumesema kwamba sheria hii itajulikana kama ni sheria ya mahakama ya biashara ya Zanzibar, yaani ni *division* ya Mahakama Kuu. Kwa hivyo, mahakama hii ya biashara ni sehemu moja ya mahakama kuu, kwa sababu ni sehemu moja ya mahakama kuu, kwa hivyo wale wafanyakazi wake, Jaji na Jaji anatoka mule mahakama kuu na wafanyakazi wengine. Hawa wote ni wafanyakazi wa mahakama na watachukuliwa kama ni wafanyakazi wa mahakama.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine la kifungu cha 11 ambalo lilizungumzia daftari. Ni kweli daftari lilizungumzwa sana. Niseme kwamba mahakama inaweza kuanzisha daftari litakalojulikana kama daftari la kesi za biashara, ambalo maelezo kuhusiana na kesi kama yanavyoweza kupokelewa kwa Mrajis. Huu ni utaratibu wa kawaida tu Mhe. Naibu Spika, kwamba kesi zinapokwenda basi mtu anayehusika anapokea kesi ile na anaiwekea kumbukumbu vizuri. Kwa hivyo, itakuwa hakuna udanganyifu tena kwamba kama kesi ilikwenda, kesi haikwenda au kama kuna mtu alikwenda kupeleka kesi au hakwenda, kwa sababu daftari lipo na kumbukumbu zitaonekana, kwa hivyo itakuwa ni ushahidi kamili kwamba kesi ile ilipelekwa lini na saa ngapi. Kwa hivyo, ni vizuri katika shughuli kama hizi kuwa na daftari maalum ambalo linaweka kumbukumbu za kesi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mchangiaji mwengine alizungumzia kuhusu kifungu cha 13 ambacho kinazungumzia uwezo wa kutoa amri na maelekezo. Suala hili Mhe. Naibu Spika, ni suala la kawaida katika mahakama. Kwa mfano unapopeleka kesi mahakamani na hakimu akaitizama ile kesi, basi hakimu ana uwezo wa kutoa maelekezo ambapo maelekezo hayo yatakuwa katika njia ya amri, ili kesi ile ifanywe nini, isikilizwe vipi au itolewe kwa utaratibu gani.

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni zuri kufanywa katika kesi kama hizi, kwa sababu hili lote linasaidia kupunguza ule wakati ambao wale wafanyabiashara wanaopigania. Kwa sababu lengo hasa la kuanzishwa kwa mahakama hizi ni

kupunguza wakati mkubwa ambao ulikuwa unazorotesha kazi au unawavunja moyo wafanyabiashara, ikiwa watakwenda katika mahakama za kawaida. Kwa hivyo, mahakama hizi zimejaribu sana kupunguza wakati na kupunguza urasimu wa kusikiliza kesi zenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ambacho kilizungumzwa ni kifungu cha 14, 16, 17. Walikuwa wanauliza hii mikutano kabla ya kusikilizwa kesi, halafu kujulishwa juu ya mkutano kabla ya kusikiliza kesi na mambo kama hayo. Wakasema je kuna umuhimu gani wa vifungu kama hivi.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu sana vifungu kama hivi kuwepo katika suala kama hili na utaratibu huu wa kukutana na wadai na wadaiwa ni mzuri, kwa sababu kesi inaweza ikawa ni kubwa sana na ikawa ina mambo mengi. Mdai anaweza kuwa anamlalamikia mdaiwa kwa mambo matano kwa mfano. Kwa hivyo, akayaandika kwamba lalamiko langu juu ya mdaiwa huyu ni hili (a), (b), (c), (d) na (e). Sasa mahakama inapowaita na wote wawili wakawepo wakakaa pamoja; wao mdaiwa na mdai pamoja na hakimu au na Jaji watazungumza na watakubaliana kwamba katika madai haya, pengine yule mdaiwa katika mambo matano yale mawili anayakubali, lakini hayakubali matatu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo kama hivyo ndivyo, yule mdaiwa atasema. Mimi la kwanza na la nne nalikubali, kwa hivyo kama la kwanza na la nne unalikubali sasa tukubaliane hivi. Hivyo wakishakukubaliana na ikiwa yale mengine matatu hawakuyakubali, hivyo yale ndio yatakayofanya kesi. Kwa hivyo, hapo ni hata ule muda wa kesi nao umeshapunguzwa. Yaani sasa kesi itasikiliza mambo matatu, wakati mwanzo kesi ingesikiliza mambo zaidi ya matano pengine.

Mhe. Naibu Spika, hii umuhimu wake ni kwamba hurahisisha mambo kwa kuyatoa yale waliyokubaliana na kuyatatua mambo ambayo ufumbuzi wake unawezekana kupatikana. Pia hufanya kesi ziende haraka, kwa sababu yale mambo yameshapunguzwa, kwa hivyo ni rahisi zile kesi kwenda haraka haraka.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa utaratibu wote huu haukukamilika au hawakufahamiana, kwa hivyo kifungu cha 18 ndicho kinachoanzisha sasa kusikilizwa kwa kesi yenyewe. Hapa kuna Waheshimiwa Wajumbe waliuliza ni nini maana ya wadawa, tafsiri yake. Kwa kweli wadawa katika kesi za *civil* za hulukia, wadawa ni watu wawili ambao mmoja ni mdai na mwengine ni mdaiwa. Kwa hivyo, wale wanapopeleka kesi katika mahakama hizi, kwa hivyo wale huitwa ni wadawa. Mmoja anakuwa ni mdaiwa na mwengine anakuwa ni mdai. Kwa hivyo, kwa ujumla wote hawa ndio wadawa.

Kifungu cha 24 kinazungumzia sana suala la usiri na ni vyema, kwa sababu hapa hii kesi bado haijenda mahakamani na kwa sababu kesi haijenda mahakamani, ni Jaji tu anayehusika akawaita wadawa, mdai na mdaiwa wakakaa na kukubaliana baadhi ya mambo na mengine hawakukubaliana. Kwa hivyo, mambo yale ni lazima yawe siri kwanza mpaka hapo yatakapomalizika, kwa hivyo pale yanaweza kuwa sio siri tena. Ni vizuri kuweka siri katika masuala haya kabla hayajatoka nje na kuharibu utaratibu mzima wa uendeshaji wa mahakama.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo lilizungumzwa liko katika kifungu cha 30, hili linazungumzia suala la lugha. Waheshimiwa Wajumbe walisema kwamba lugha yetu ni ya Kiswahili na kwa nini sasa tukasema lugha ya mahakama hii ama itakuwa Kiswahili au itakuwa Kiingereza, na kumbukumbu ziwekwe kwa lugha ya Kiingereza.

Mhe. Naibu Spika, ni suala zuri, lakini ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wakajua tu kwamba suala la mahakama kidogo ni suala ambalo linaingilia mambo ya Kimataifa. Mhe. Naibu Spika, tujalie kwamba mdai au mdaiwa ni mtu kutoka nje Ujerumani, ana biashara zake hapa, amekorofishana kidogo hapa na watu wengine, au pengine wao wenyewe Mjerumani na Mjerumani au Mjerumani na Muitaly, vyovyote vile tutakavyotoa mifano. Lakini kwa sababu ile kesi iko hapa, madai yale yako hapa. Kwa hivyo ni lazima ile kesi itakwenda katika mahakama za Zanzibar. Sasa kumbukumbu ambazo zitawekwa ni lazima ziwekwe katika lugha ambayo, hata wale wakitaka kuchukua zile kumbukumbu au wao wakitaka kukata rufaa wawe hawana matatizo na ndio maana tukasema kwamba ni vizuri kwa kesi kama hizi zikaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili au ya Kiingereza.

Mhe. Naibu Spika, lile dai ya kusema kwamba watu wetu pengine hawajui lugha na kadhalika. Nakubaliana na kwamba watu wetu hawajui lugha ya Kiingereza, lakini hatua inapofikia kesi kama hapa ambayo ni ya mamilioni ya pesa, hata kama ni mtu wetu, hatokwenda yeye mahakamani atamtafuta Wakili mzuri na wakili huyo ndiye atakaye muwakilisha Mahakamani. Sasa akifanya hivyo kutakuwa kuna Wakili wa mdai na Wakili wa mdaiwa, hawa ndio watakaozungumzia ile kesi na katika mazungumzo yao bila shaka watazungumza kwa mujibu wa utaratibu wa

uendeshaji wa kesi ulivyowekwa. Kwa hivyo, sisi tulikuwa hatuoni haja kubwa sana ya kusema kwamba lazima tutumie lugha ya Kiswahili. Tutumie lugha ya Kiswahili pale ambapo pengine wadaiwa wote ni wa hapa hapa, kwa sababu zile kumbukumbu baadae unaweza ukapeleka katika mahakama ya rufaa. Kwa hivyo, ni vizuri zikawa kwa Kiingereza ili unapopeleka katika mahakama ya rufaa iwe na urahisi wa kuzisikiliza kesi zile. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana Waheshimiwa Wajumbe waone umuhimu huo wa kuweka kumbukumbu hizi kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu hiyo.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa lipo katika kifungu cha 31 na hapa nina ushahidi kwa njia ya *video*. Kuna Mheshimiwa mmoja alisema kwamba je, kuna haja gani ya kuwa na ushahidi kwa njia ya *video* hii. Utaratibu wa siku hizi Mhe. Naibu Spika, wanaita *conference* hizi wanaita *video conference*. *Video conference* ni kwamba wewe uko nchi moja na yule unayemuhitajia kwa masuala fulani yuko nchi nyengine. Sasa kuja kwake pengine inaweza kuwa ni vigumu. Sasa katika kesi kama hizi Mhe. Naibu Spika, pengine anamtaka shahidi ambaye yuko Marekani, lakini ukimchukua shahidi yule ni mfanyabiashara, kwa sababu wa lile tendo lilipotokea na yeye alikuwepo hapa. Sasa unajua wenzetu wanathamini sana wakati wao na biashara zao. Unapomchukua kutoka Marekani mpaka hapa kwa kuja kutoa ushahidi, ni lazima umlipie nauli ya ndege kwenda na kurudi, nauli ya malazi na gharama zake pengine alizopoteza kwa siku zile ambazo yeye atakuwa hayupo kule.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ili kuyakinga hayo, basi ushahidi wa *video* kama huu unakubalika. Lakini huyo anayeomba ushahidi kwa njia hii ni lazima agharamie gharama zote ambazo zitahitajika. Kwa namna gani, mahakamani pale itabidi kuwe *arranged* kwa utaratibu maalum, ili yule shahidi aliyekuwa kule nje aambiwe wakati fulani tutakupigia simu, uwepo kwenye simu, utaulizwa maswali ujibu. Sasa ukifanya hivyo, angalau zile gharama za kumuita yule shahidi kuja katika kesi zinapungua na ndio maana tukasema katika sheria hii kuwa ushahidi wa namna hiyo pia nao utaruhusika, kwa sababu ni ushahidi ambao nyinyi mnamsikia na nyote mpo, mnamuuliza maswali na baada ya kumaliza, mwengine anaweza kumuuliza tena maswali kwa utaratibu wa kimahakama. Kwa hivyo, hii nayo inapunguza hata zile siku za kesi. Kwa sababu kama ukilazimisha kwamba yeye aje huku, anaweza kukuambia mwezi huu mimi sina nafasi kwa sababu nina kazi hii na hii, au labda mnilipe kiasi hiki ndio nije, basi mimi nitakuja mwezi wa 8 pengine ndio nafasi yangu. Kwa hivyo, kesi itachelewa na lengo hapa ni kuzifanya hizi kesi ziende haraka haraka. Ndio maana tukasema *video conference* zitakubalika na zitachukuliwa kama ni ushahidi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililozungumzwa liko katika kifungu cha 40, ambacho kinatoa uwezo kwa Jaji Mkuu kuunda kanuni kwa ajili ya mambo ambayo yametajwa. Sasa mwengine akasema kwa nini tukasema kwamba Jaji Mkuu anaweza, kwa nini hatukusema kwamba Jaji Mkuu atatunga kanuni.

Kiuandishi neno zuri ni kwamba anaweza, kwa sababu anaweza halimlazimishi kwamba wakati wowote atunge kanuni, isipokuwa pale ambapo pana haja, basi Jaji Mkuu anaweza akatunga kanuni. Lakini ukisema Jaji Mkuu atatunga kanuni, ina maana kwamba Jaji Mkuu ni lazima atunge kanuni, hata kama hakuna haja ya kufanya hivyo. Kwa hivyo, huu ni uandishi tu wa kisheria ambao unamruhusu Jaji Mkuu kufanya chochote kile katika suala la kutunga kanuni pale ambapo anahisi kwamba kuna haja ya kufanya hivyo.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, niliulizwa kwamba kuna Jaji Mkuu anaweza kutunga kanuni. Lakini pia kuna Waziri anaweza kwa amri iliyochapishwa katika gazeti rasmi kutunga kanuni vile vile. Sasa je, kanuni hizi hazitagongana baina ya Jaji Mkuu na Waziri.

Kwa hivyo, naomba hapa ieleweke kwamba Jaji Mkuu Kanuni ambazo mara nyingi anatunga ni zile Kanuni ambazo za *Administrative rules* ambazo ziko katika Mahakama zile ni mamlaka ya Jaji Mkuu kutunga Kanuni hizo na wala Waziri hawezi kutunga hizo.

Lakini Waziri anaweza kutunga Kanuni za utekelezaji mzuri wa ile Sheria yenyewe. Kwa mfano, waziri anaweza kutunga Kanuni akasema sheria hii sasa lazima ikitaka kusikilizwa kuwe kuna mambo haya na yale yapatikane lakini zile shughuli hasa za utendaji ndani ya Mahakama zile hazimuhusu Waziri na hiyo ni kazi ya Jaji Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, Kanuni hizi za watu wawili hawa hazitagongana wala hazitafanya utekelezaji wa sheria hii kuwa na matatizo.

Mhe. Subeit Khamis Faki naye pia alizungumzia kuhusu kifungu cha 36 na 39, vifungu hivi utaona vina maneno ya x. Kwa mfano, kifungu cha 36 kuna xxix, hii kwa lugha nyengine ni 29. Sasa akasema kwa nini tuseme amri hivi tusiseme tu.

Mhe. Naibu Spika, amri hii ni amri ambayo iko katika Kanuni za Mwenendo wa Madai, ambao kwa Sheria zetu ni Sura ya 8 ya Sheria za Zanzibar. Sasa Kanuni zile zimegaiwa katika utaratibu huu ukisema tu amri kwa mfano ya 29, basi unajua amri ya 29 inahusiana na viapo pamoja na mambo kama hayo. Kwa hivyo, hapa ni sawa na kusema bila ya kujali sharti la amri ya 29 ya mwenendo wa madai, yaani hiyo amri ya viapo na mambo mengine kama hayo.

Lakini hapa hatuwezi kuandika tu amri hiyo iko katika sura gani, isipokuwa tayari tumeshaandika tu amri ya 29 ya Sheria ya Mwenendo wa Madai, basi inajulikana, hali kadhalika na ile amri nyengine ya 22 ambayo inazungumzia masuala ya *security for cost* na mambo kama hayo. Kwa maana hiyo, huu ni utaratibu tu wa uandikaji wa sheria hizi, kwa maana hiyo hakuna matatizo ya kuziweka kama hivi zilivyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo tunao ufafanuzi mwengine mdogo, ambao ningelipenda niuzungumze, ambapo katika kifungu cha 5(3) alisema kwamba fedha hizi ni nyingi au kiwango ni kikubwa sana na kipunguzwe, yaani alisema kwamba shilingi milioni 30 iwe milioni 20 na milioni 20 iwe milioni 10 na alitoa sababu kuwa wafanyabiashara wengi hawana uwezo huo.

Kwa kweli kwamba kiwango ni kikubwa. Lakini kwa mujibu wa kesi kama hizi kiwango cha milioni 30 Mhe. Naibu Spika, na kiwango cha milioni 20 kwa kesi kama hizi tunahisi si kikubwa, kwa sababu kesi hizi zina-*involve* madai makubwa pamoja na gharama nyingi, kwa hivyo tukiweka kidogo basi hizi kesi tutafanya na kwanza inategemea.

Lakini nadhani tunapoweka kiwango kama hichi cha kufanya kwamba ile ndio Mahakama ya Biashara kwa hiyo zile kesi ambazo zitakwenda kwenye Mahakama ile basi zitakuwa ni chache na zitasikilizwa kwa wakati muafaka, lakini tukipunguza kiwango nahisi tutaingiza kesi nyingi ambazo pengine nyengine hazina haja ya kwenda katika Mahakama hizo za Biashara.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri kiwango hichi kitasaidia sana katika kuzipunguza zile kesi na kujua kuwa kesi hizi zinakwenda katika Mahakama ya Biashara na zinapokwenda ni kesi ambazo lazima zishughulikiwe kwa haraka tena inavyowezekana.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Naibu Spika natumai mengi nimeyajibu pia Waheshimiwa Wajumbe wengi kama nilivyosema mwanzo walijaribu au waliupongeza sana mswada huu na walitoa mapendekezo na sasa mapendekezo yale.

Mhe. Naibu Spika naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutayachukua na kuyafanyia kazi, ili tuweze kuufanya mswada huu uwe mzuri zaidi kwa ajili ya lile lengo la kusema kwamba kesi hizi sasa zishughulikiwe haraka, ili wafanyabiashara wasivunjike moyo waweze kubakia hapa na wasiende kwenye maeneo mengine kufanya biashara waweze kubakia, na nchi yetu Zanzibar iweze kufaidika kutokana na wafanyabiashara hao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wakubali mswada huu, ili uweze kupitishwa na mwisho uweze kuwa ni sheria, ili Mahakama yetu ya Biashara iweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.
Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja kwa hivyo nitawahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, sasa anaomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahakama Kuu) ya 2013

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.
Kifungu 2 Matumizi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 3 Tafsiri pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili

Masharti ya Uendeshaji

Kifungu 4 Kuanzishwa kwa Mahakama ya Biashara.
Kifungu 5 Mamlaka ya Mahakama pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6 Muundo wa Mahakama pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 7

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati nilipokuwa nikichangia katika kifungu hichi cha 7(1) Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 7(1) kinaeleza hivi:-

> "Kutakuwa na Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara ambayo itajumuisha Majaji wa Mahakama ya Biashara, Wakili mmoja anaeteuliwa na Jumuia ya Wanasheria wa Zanzibar, Wakili wa Serikali atakayeteuliwa na Mwanasheria Mkuu, mtu mmoja atayeteuliwa na Mwanasheria Mkuu, mtu mmoja atayeteuliwa na Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima wa Zanzibar na mwakilishi mmoja kutoka Wizara inayohusika na Biashara".

Mhe. Mwenyekiti, nilimuomba Mhe. Waziri hapa kuwa angalau hapa pawe na mwanamke mmoja kwa sababu hawa kila mmoja anateuliwa na mtu wake. Sasa pangekuwa na *tanbihi* hapa Mhe. Naibu Spika hapa angalau mwanamke mmoja akawemo kwenye kifungu hichi na wala sikusikia Mhe. Waziri kunijibu kwamba inawezekana au haiwezekani, Mhe. Naibu Spika naomba jibu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Mwakilishi alizungumzia kuwepo kwa mwanamke mmoja. Lakini Mhe. Mwenyekiti ukitizama hii Kamati yenyewe, yaani Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara, ambayo itajumuisha Majaji wa Mahakama ya Biashara.

Sasa hawa Majaji wanatoka Mahakama Kuu na wapo majaji wawili wanawake hivi sasa, ukitizama mawakili Jumuia ya Wanasheria wapo wanawake pia, ukitizama wafanyabiashara wa Zanzibar wanawake ndio wengi, na ukitizama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wanawake wapo. Lakini kwa upande wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko sina uhakika kwamba mwanasheria ni mwanamke au vipi, lakini hizi taasisi nyengine zote wanawake wamo.

Kwa hivyo, ni jukumu la hawa viongozi wa taasisi nao kuona kwamba wanawake wanapata nafasi kama hiyo, sasa tukiweka hapa kwamba na mwanamke mmoja tunaweza kupata matatizo mwanamke mmoja kutoka sehemu gani, kwa sababu hapa tunazungumzia mambo ya biashara na hawa wote utaona wanahusiana na mambo ya kibiashara.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana tuwaachie viongozi hawa wakuu ambao wana busara na pia wanajua siku hizi kuna *gender*, basi naamini kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu, Jaji Mkuu, wafanyabiashara pamoja na wanasheria hawa watakaa pamoja kutizama kwamba mwanamke na yeye anafaa, ili aweze kuwa mjumbe wa kamati hii. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri ameshalizungumza kuwa watakaa pamoja wakubaliane ni upande gani atolewe mwanamke. Kwa hiyo, naomba tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, jana nilichangia kifungu hichi na nilihoji kwamba Kamati ya Watumiaji kwanza kuna sehemu inasema Majaji wa Mahakama ya Biashara, niliomba kujua ni wangapi wawili, watatu, hamsini au mia moja, kwa sababu wajumbe wengine wote wametajwa mmoja au wawili, lakini hawa ni wangapi.

Vile vile nilisema hapa kwamba wengi hapa wajumbe hawa ni wawakilishi wa serikali na wananchi wa kawaida watakuwa wamewakilishwa na mjumbe mmoja wa Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima. Sasa uwakilishi wa raia utakuwa ni mdogo zaidi kuliko wale wafanyakazi wa Mahakama.

Kwa hivyo, naomba kupatiwa ufafanuzi ni majaji wangapi watakaotengwa hapa, lakini kwa nini wananchi wakawakilishwa na mtu mmoja tu na wengine wote wakabakia kwenye mahakama. Je, itakuwa ni Kamati ya Watumiaji au Kamati ya Mahakama.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, sijasikia vizuri naomba arudie Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba urudie tena Mhe. Waziri hakusikia vizuri, kwa sababu umesema lakini hakufahamu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza ni kwamba kifungu cha 7(1) ambapo, Kutakuwa na Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara, ambayo itajumuisha Majaji wa Mahakama ya Biashara. Kwa hivyo, ningeomba kujua ni wangapi wawili, watatu.

Vile vile nilisema kwamba hii kamati itakuwa na wajumbe wengi, lakini wengi wao ni wanasheria na majaji, lakini mjumbe mmoja tu ndiye ambaye atatokana na Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima ya Zanzibar. Sasa nikaomba hapa kungekuwa na uwiano baina ya wale majaji na wale wajumbe wengine, ili kuifanya ile kamati kuwa na uwezo zaidi wa kutetea watu wengi na hivi ilivyo hii kamati itakuwa zaidi ya wanasheria na majaji.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mjumbe, kwanza swali lake la mwanzo kusema kwamba hawa Majaji wa Mahakama ya Biashara ni wangapi hivi sasa hatuwezi kusema, kwa sababu idadi ya Majaji hawa itategemea ukuaji wa ile mahakama yenyewe, kama vile tunaweza kufungua mahakama hivi sasa na kuwa na jaji mmoja, lakini kama kesi zitazidi basi tunaona kwamba kuna haja ya kuongeza jaji na wakawa majaji wawili.

Kwa hivyo, hapo wataingia kutokana na ule uzito wa zile kesi zilizopo na wale majaji ambao wameteuliwa, na ndio maana hatukusema kama ni jaji mmoja au wawili ama watatu na wala haiwezi kuwa majaji watatu na wawili ni nadra sana, na hatukusema hivyo kwa sababu hiyo.

Swali la pili ukitizama hizi ni kesi za biashara ndio madhumuni ya mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hiyo ndio nikasema Wakili mmoja atateuliwa na Jumuia ya Wanasheria, Wakili wa Serikali atakayeteuliwa na Mwanasheria Mkuu na Jumuia ya Wafanyabiashara itateua mmoja na mwakilishi mmoja wa wizara inayohusika na biashara.

Kwa hivyo, wote hao utaona ni watu wanaohusiana na suala hili na hawa lengo lao hii kamati kama ukisoma hichi kifungu cha 6 Mahakama hiyo itakayokuwa ya Biashara itakuwa na Jaji na halafu itakuwa na watu wawili ambao hawa ndio watakaowateua, kwa sababu hawa wanakaa, ili kuteua hao Washauri wa Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri haina haja sana kuwa na watu wengi na kuwa na uwakilishi kutoka sehemu nyingi, kwa sababu wote hawa wawakilishi hapa kwenye kifungu cha 7 ni watu ambao wanahusiana na suala la biashara na hao wangewateua watu wawili hao kuwa ni washauri wa huyo Jaji ambaye atasikiliza kesi za biashara.

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Mjumbe akubali *composition* hii ya kamati, ili wao ndio waweze kuteua kwa pamoja nani na nani atakuwa mshauri mzuri katika kesi hizi za biashara. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa Mhe. Waziri, lakini bado nina mashaka au vyenginevyo sijafahamu hichi Kiswahili. Kwa kweli Kamati hii ni ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara, kwamba wale watumiaji wenyewe wa Mahakama ya Biashara watakuwa na kamati yao, ambapo *composition* yake itakuwa miongoni mwa Wajumbe; ni Majaji wa Mahakama ya Biashara na Mhe. Waziri amekiri hapa kwamba hajajua idadi, sasa inawezekana itakuwa wawili ama kwa mwenendo wa serikali ulivyo wanaweza kuwa 10. Lakini bado *composition* ya wajumbe wengine kutoka Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima atakuwa ni mtu mmoja.

Sasa serikali ikiamua hawa majaji wawe 10, basi watakuwa 10 kwa sababu ndivyo sheria ilivyosema, lakini hii ni Kamati ya Watumiaji na watumiaji hawa zaidi ni wale wafanyabiashara wenyewe, ambao watakaa zaidi kwa ajili ya kufanya suluhu na kuwachagua wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini majaji tusiwataje kama vile wawili au watatu, lakini kuweka wazi hivi maana yake tunaweza kusema wawe 10, ili wakati wajumbe wa Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima ni mtu mmoja.

Kwa hivyo, nadhani hili Mhe. Waziri alizingatie zaidi kwa maslahi ya wafanyabiashara au vyenginevyo labda sijafahamu hichi Kiswahili cha Kamati ya Watumiaji.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimtoe wasi wasi Mhe. Mjumbe kwamba majaji hawa hawatakuwa 10. Kwa hivyo, kwa sababu hii ni Mahakama ya Biashara, itaanzishwa na ikishaanzishwa basi anaweza kuteuliwa jaji mmoja na huyu ndiye atakayekuwa mjumbe wa hii kamati. Lakini kama kesi za biashara zitakuwa nyingi na zitalazimisha kuongeza jaji basi wanaweza kuwa majaji wawili.

Vile vile kesi za biashara kubwa kama hizi hazitakuwa nyingi kiasi cha kufanya Mahakama ziwe mbili za Biashara na mara nyingi jaji atakuwa ni mmoja ndio lengo la hapa. Mhe. Mwenyekiti, hata kama watakuwa ni majaji wawili, basi lengo hapa ni kutizama na kutoa au kutizama zile kesi zenyewe zinakwenda vipi na matatizo yako wapi.

Kutokana na hali hiyo, hata wale majaji wawe wawili kwa mfano, basi kutakuwa na umuhimu wa kuwepo katika ile kamati kwa ajili ya kujadili namna gani ya kutatua matatizo yale ya kibiashara ili kesi hizi za kibiashara ziweze kwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba Jaji au Majaji wa Mahakama ya Biashara hawa inategemea zile kesi zenyewe zitakuwa ngapi na uteuzi wenyewe utakuwa vipi, isipokuwa Mahakama ya Biashara itakuwa ni moja na ikiwa moja basi Jaji atakuwa ni mmoja, mpaka pale kama kuna *volumes* nyingi za kesi na ile *load* ni kubwa sana na Jaji Mkuu akasema sasa tuteue Jaji mwengine inaweza ikawa hivyo, lakini ni nadra sana.

Kwa hivyo, *composition* itakuwa kama hivi kama vile Jaji mmoja, Wakili mmoja, Mwanasheria mmoja kutoka Wizara ya Biashara mmoja na mwakilishi wa Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima ni mmoja na hiyo ndio itakuwa ni *composition*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, labda nikubali ingawa Mhe. Waziri anazidi kunizonga, lakini naomba kuweka indhari kwamba Jaji Mkuu atakapoamua kwamba kesi zimekuwa nyingi maana yake atapanua wigo wa Mahakama ya Biashara, lakini bado mwakilishi wa Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima ni mmoja, sasa napata mashaka tutamgawa vipi kuwakilisha hizi mahakama. Lakini naomba tuendelee na itakuwa yeye mwenyewe anajua undani wake na mimi nadhani napata mashaka kidogo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante wakati nilipokuwa nachangia mswada huu wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria nilitaka ufafanuzi zaidi juu ya Kamati ya Watumiaji na kidogo jambo lililonitatiza ni kwamba kwenye Muundo wa Mahakama, ambao unazungumzia kwamba kutakuwa na Jaji ambaye anayeteuliwa na Jaji Mkuu na washauri wawili kutokana na hawa wajumbe wa Kamati ya Watumiaji, sasa hapa kidogo pamenitatiza.

Kwa hivyo, nataka kujua kwamba hii Kamati ya Watumiaji itakuwa inafanya kazi wakati gani na tukiangalia huu Muundo wa mahakama ya Biashara itakuwa na wajumbe watatu, yaani mmoja ni huyu Jaji na washauri wawili, sasa hawa washauri watatokana na hawa wajumbe wa Kamati ya Watumiaji na hapa kidogo pamenipa mashaka.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi tukizingatia kwamba hii Kamati ya Watumiaji itakuwa inaishauri Mahakama ya Biashara kuhusu mambo ya utendaji pamoja na mambo mengine ya kuwasilisha orodha ya watu wenye uelewa kwa mujibu wa kifungu cha 7(3).

Mhe. Waziri namuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba atupe hasa huu Muundo wa hii Mahakama ya Biashara utakuwaje na hii Kamati ya Watumiaji, kwa sababu naona kama inajirejea. Kwa mfano, kwenye kifungu cha 6(a) na (b) vinazungumzia muundo, naomba kunukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 6(a) na (b) kinaeleza hivi:-

> 6. Mahakama itajumuisha:
> (a) "Jaji atakayeteuliwa na Jaji Mkuu miongoni mwa majaji wa Mahakama Kuu au Hakimu wa Mkoa aliyekasimiwa mamlaka ya ziada ya kusikiliza migogoro ya Biashara na atakuwa ndiye Mwenyekiti;
> (b) Washauri wawili miongoni mwa watu walioteuliwa na Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nahitaji kupata ufafanuzi kuhusu huu muundo hasa wa Mahakama ya Biashara utakuwa vipi na zaidi ukizingatia kwamba cha 7(2), ambapo naomba kunukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 7(2) kinaeleza hivi:-

> "Jaji dhamana wa Mahakama ya Biashara atakuwa Mwenyekiti na Mrajis atakuwa Katibu wa Kamati".

Sasa naomba kidogo Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti atupe ufafanuzi juu ya Muundo wa Mahakama yenyewe na hii Kamati ya Watumiaji itafanya kazi wakati gani ukizingatia kwamba kuna wajumbe wawili na wao watakuwa wanaungana na Jaji ambaye anayeteuliwa na Jaji Mkuu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Mjumbe alizungumzia kifungu cha 6 na 7. Kifungu cha 6 kinaelezea kuhusu ile *composition* ya mahakama itakuwa ni Jaji pamoja na washauri wawili na hii ndio Jopo la Mahakama litakalisikiliza zile kesi.

Sasa hawa washauri wawili watapatikana vipi, watapatikana katika kifungu cha 7, ambapo kuna Kamati ya Watumiaji ambao wamewekwa pale, hawa watakaa na kuamua watateua watu wawili kuwa ni washauri wa huyo Jaji, yaani hii kamati ndiyo itakayokaa na kusema kwamba fulani na fulani ndio watakaokuwa washauri wa Jaji katika kesi hii.

Swali la pili ni kwamba Jaji dhamana wa Mahakama ya Biashara atakuwa Mwenyekiti na Mrajis atakuwa Katibu wa Kamati. Sasa ukitizama Mrajis anatoka wapi, ukitizama tafsiri mrajis, maana yake ni Naibu Mrajis wa Mahakama ya Biashara na itajumuisha mtu yeyote anayekaimu uwezo huo. Kwa hivyo, kutakuwa na Mrajis ambaye atateuliwa, anayeshughulikia na mambo ya Mahakama ya Biashara kwa hiyo huyo ndiye atakayekuwa Katibu na hilo ni suala jengine.

Lakini kifungu cha 3 kinaeleza kwamba itakuwa ni jukumu la Kamati ya Watumiaji, yaani hawa watu walioteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 7(1), ambapo ni Jaji, Mwanasheria mmoja, mwakilishi mmoja kutoka Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima na watu kama hao. Sasa hao watakaa kwa ajili ya kumshauri Jaji wa Mahakama ya Biashara kuhusu mambo ya utendaji wa mahakama na kuwasilisha orodha ya watu wenye uelewa wa mambo ya biashara.
Kwa hivyo, hawa watashauri ile mahakama, lakini pia wao wanaweza kukaa na kusema kwamba fulani ni mzuri kwa mambo ya biashara na kuweka *list* yao pale na kumwambia Jaji kuwa *list* hii ndio watu tunaohisi kwamba wao

wanaweza kuchukuliwa kwenye jopo ambalo litasikiliza kesi za biashara na itakuwa *list* ipo wanachukuliwa wawili na huu ndio utaratibu.

Kwa maana hiyo, kamati hii kazi yake ni kushauri na kutafuta wale washauri wa kusikiliza kesi. Mhe. Mwenyekiti, hii zaidi utekelezaji wake utakuweko huko tulikosema kwamba Jaji Mkuu ataweka utaratibu, yaani Kanuni kwa sababu sheria lazima kuwe na Kanuni za utaratibu gani watafanya ili masuala haya yaweze kutendeka. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, imeeleweka.

Kifungu 7 Kamati ya Utumiaji wa Mahakama ya Baashara
Kifungu 8 Wafanyakazi wa Mahakama pomoja na marekebisho yake
Kifungu 9 Vikao vya Mahakama Pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA TATU

Ufunguaji wa Kesi

Kifungu 10 Ufunguaji Mashauri Pamaja na Marekebisho yake
Kifungu 11 Daftari la Kesi Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 12 Kupangiwa kwa Kesi Pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA NNE

Kupanga Kesi Kabla ya Kusikilizwa na Mkutano

Kifungu 13 Uwezo wa Kutoa Amri na Maelekezo Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 14 Mkutano wa Kabla ya Kusikilizwa Kesi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 15 Kujulishwa Juu ya Mkutano wa Kabla ya Kusikilizwa Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 16 Kushindwa Kuhudhuria kwa Upande Mmoja au Zaidi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 17 Uharakishwaji Kesi Pamoja na Marekebisho Yake.

SEHEMU YA TANO

Usuluhishi

Kifungu 18 Kuwasilisha kwa Ajili ya Usuluhishi
Kifungu 19 Kuhudhuria Usuluhishi
Kifungu 20 Mamlaka ya Kutatua Jambo
Kifungu 21 Kushindwa Kuhudhuria kwa Mdawa Katika Usuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 22 Kurejesha Kesi Iliyofutwa kwa kushindwa kuhudhuria Usuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 23 Wajibu wa Msuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 24 Usiri
Kifungu 25 Muda wa Usuluhishi
Kifungu 26 Mwisho wa Ushuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 27 Kushindwa Kufikia Suluhu kwa Njia ya Usuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 28 Washauri
Kifungu 29 Ushahidi wa Kiapo kwa kesi iliyoanza kwa *Originating Summons* Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 30 Lugha ya Mahakama.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia Mswada huu wa Mhe. Waziri nilizungumzia juu ya lugha ya Mahakama hii ya Biashara ambapo Mswada unasema kwamba miyenendo yote ya Mahakama itanakiliwa kwa Kiingereza. Sasa nilikuwa nahitaji ufafanuzi kwa nini hii mienendo ya Mahakama inakiliwe kwa kiingereza wakati lugha rasmi ya Taifa ya Tanzania ni Kiswahili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, wakati nilipokuwa nikijumuisha nilisema kwamba ni kweli lugha ya Mahakama itakuwa ama Kiswahili au kiingereza. Isipokuwa miyenendo yote Mahakamani itanakiliwa kwa kiingereza. Hapa Mhe. Mwenyekiti hatukufunga kwa sababu zile kesi inaweza ikawa ni wenye kudaiyana (wadau) mtai na mdaiwa, wanaweza wakawa wote ni waswahili wa hapa hapa kwa hivyo inaweza ikaendeshwa kwa Kiswahili. Lakini kesi za biashara kubwa kama hizi mara nyingi zina *involve* watu kutoka nje.
Tuchukue mfano kuna hoteli fulani labda ya Kiwengwa wamegombana na Hoteli fulani iliyiokuwepo Nungwi, wote ni wageni. Sasa pale ukisema lazima iende kwa Kiswahili itakuwa sivyo. Ndio tukasema kwamba ama iende kwa Kiswahili au kiingereza, haya ndio madhumuni makubwa. Lakini Kiswahili hukatazwi unaweza ukasema na kiingereza unaweza ukasema hasa kama hawa wadau wote ni watu ambao hawajui Kiswahili. Madhani hii kesi tumeianzisha hapa ni lazima tutapata wadau wa aina hii, watagombana wao wenyewe kule hata sisi wenyewe waswahili hatumo. Kwa hivyo wakija pale huwezi kuwambia lazima muendeshe kwa Kiswahili itakuwa sivyo. Ndio maana tukasema inaweza ikawa kwa Kiswahili au kwa kiingereza. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimemuelewa isipokuwa tatizo langu moja kama ataliweka sawa hilo basi nitakuwa sina tatizo. Tatizo langu ni hii isipokuwa, kwa sababu inasema kwamba lugha ya Mahakama itakuwa ama Kiswahili au kiingereza kwa hapo sina tatizo. Lakini isipokuwa kwamba mienendo yote ya Mahakamani itanakiliwa kwa kiingereza. Maana yake kwamba mienendo ya Mahakamani itakuwa inanakiliwa kwa lugha ya kiingereza. Sasa kwa nini isiwe na Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri umemfahamu?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Nimemfahamu Mhe. Mwenyekiti. Ni kweli tumesema kwamba ile mienendo yenyewe itanakiliwa kwa kiingereza. Hii kuna sababu, kwa sababu hii ni Mhakama kubwa lakini kuna nafasi za kukata rufaa kwanza. Kwa sababu kuna nafasi hizo na huko kwenye Mahakama za Rufaa wanachotumia ni kiingereza tu, kwa hivyo zile *proceedings* kama zipo kwa kiingereza itakuwa ni urahisi, hilo la kwanza.

La pili proceedings zinaweza zikachukua files zima kama hivi sasa ukikata rufaa ukianza kutafsiri itachukua muda na lengo ni kuwalinda hao wafanyaiashara kupunguza muda mrefu. Sasa ikiwa imenakiliwa kwa kiingereza itakuwa ule muda nao pia umepungua.

Lakini la tatu ni ule mfano nilioutoa wa wafanyabiashara ambao sio waswahili lakini ni wa nje, wale watataka kuondoka na ma –*proceedings* yao pengine yule ana Kampuni yake nje huko kwenda kusema kwamba *proceedings* zetu ni hizi lakini mimi nimeshindwa kwa sababu hii na hii. Kwa hivyo itakuwa pia ni urahisi. Kwa hivyo tumajaribu kurahisisha huu utendaji wa Mahakama kwa misingi hiyo. Nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mimi bado ninatatizo kidogo kwa nini inakiliwe kwa kiingereza peke yake kusiwe na Kiswahili. Kwa sababu *proceedings* hizi au mienendo hii ya kesi inavyoandikwa kama mimi niko hapa hata kama kesi inakwenda nje, lakini mimi ninaeomba *proceedings* ili nifungue rufaa au nikate rufaa niko hapa, kwa hivyo kwanza natakiwa nielewe mimi, sasa kama sijui kiingereza nitajuaje ule mwenendo mzima. Kwa sababu mimi nataka *proceedings* ili sasa nikate rufaa nitakapouona mwenendo wa kesi ndio utakaonishawishi kwamba sasa nikate rufaa au nisikate rufaa. Sasa hilo suala la kwamba rufaa imeshakatwa kesi inakwenda Marekani wapi, wapi, hilo ni jengine.

Kwa hivyo *proceedings* hizi zisiwekwe mbano kwamba lazima ziandikwe kwa kiingereza. Kama mimi ninaekata rufaa sijui kiingereza kwa hivyo ni lazima kwanza mimi nifahamu mwenendo mzima wa kesi ilivyokwenda, ili unishawishi niweze kukata rufaa. Sasa ndio namwambia Mhe. Waziri isibanwe hii kwamba ikazuiliwa kwamba lazima *proceedings* iandikwe kwa kiingereza.

Hili Mhe. Mwenyekiti, tabia hii ipo sio kesi zinazokwenda nje tu, hata hizi kesi zetu za ndani, mtu anapoomba *proceedings* Mahakamani basi Hakimu anaandika kwa kiingereza na ndio sote waswahili hapa. Anaandika kwa

kiingereza anampa mtu *proceedings*, basi. Sasa ndio nazungumzia ni lazima tuwe na lugha mbili, lazima lugha yetu hii Mhe. Mwenyekiti, tuithamini, tusithamini lugha za kigeni.

Juzi Rais wa China alipokuja hapa kutembelea Tanzania kwa bahati nilikuwepo alikuwa anatuhutubia sisi Watanzania lakini alikuwa anahutubia kwa Kichina, anazungumza Kichina, kabisa na kiingereza pengine anafahamu yule lakini pale anazungumzia juu ya kuthamini lugha yao. Lakini sisi kila kitu kiingereza, kiingereza, haya ni mambo ya kikoloni haya. Kwa hivyo hizi lugha ni lazima ziwe zote mbili, tusibane kwenye sheria. iwe kiingereza au Kiswahili ili wananchi waweze kufahamu. Sasa Mhe. Waziri ukubali tusibanwe kwamba lazima proceedings iandikwe kwa kiingereza iwe pamoja na Kiswahili ili yule Mswahili anapokata rufaa basi aelewe ule mwenendo kabla ya kukata hiyo rufaa inayokwenda huko nje.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri utaratibu wa *proceedings* na Mahakamani kesi kama hii unapokwenda Mahakamani wewe mwenyewe unaedai kwa mfano unakwenda Mahakamani na umeshamchukua Wakili wako. Wakili wako ndie anayesema baina ya Jaji na Wakili na Wakili mwengine, wewe upo pale unasikiliza kila kitu, unajua kila kitu lakini yule Jaji tu yeye ndiye anaye *record* kwa kiingereza, huku wakili wako ana *record* kila kitu mnachozungumza. Kwa hivyo kuelewa unaelewa, lakini tukisema kwamba Jaji aandike kwa kiingereza halafu aandike kwa Kiswahili, huo muda utakuwa haupo na halafu inaweza ikaleta matatizo. Kwa hivyo Jaji yeye ndiye anayeambiwa kwamba aandike kwa kiingereza zile *proceedings*. Lakini huku wakili wako na wewe mwenyewe upo unasikiliza na baadae ukiridhika na yale maamuzi yaliyotoka kwa sababu utakuwa upo kwenye zile kesi siku zote utakuwa unajua kwamba hapa nimeonewa au hapa siwezi kushinda, wewe na wakili wako mtawasiliana.
Kwa hivyo hii ni *proceedings* ile ya jaji tu ili kurahisisha yale mazungumzo pale au maelezo pale. Lakini tukisema kwamba Jaji aandike kwa Kiswahili halafu aandike kwa Kiswahili halafu hapo hapo atafsiri kwa kiingereza kwanza itambabaisha.

Lakini la pili wakati mwengine kesi kubwa kama hizi wanaweza wakaja mawakili kutoka nje hawajui Kiswahili, wanazungumza, sasa wakizungumza wewe huwezi kutafsiri kwa Kiswahili halafu uandike tena kwa kiingereza. Itakuwa yote ni time ambayo tuna *consume* bure. Ndio kwa hivyo yeye Jaji tutamuachia uhuru huo. Lakini hao wengine yule mtu ambaye yupo na wakili wake watazungumza pale na watafahamiana kwa Kiswahili na mazungumza pale yatakuwa ni kwa Kiswahili na kiingereza.

Kwa hivyo mimi ningelimuomba Mhe. Salmin Awadh Salmin, akatizama kwa misingi hiyo na tunamuomba kwamba aturuhusu tuendelee na hivi. Sasa nakubali kwamba *concern* yake katika kesi pengine za jinai pengine zina makosa kama hayo au utaratibu huo si mzuri basi utaratibu huo katika kesi hizo tutakaa na kufikiria njia gani ya kufanya ili na yule aliyekuwepo pale aweze kupata kila kitu. Lakini kwa hii namuomba akubali kwa hivyo lakini hizo nyengine alizozisema za *criminal* na nyenginezo tutatizama na tutapeana ushauri kama kuna haja au tufanye vipi ili na huyu mtu wetu au wananchi yetu nayeye aweze kufaidika zaidi. Nakushukuru.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, itabidi nikubali wazo au ushauri wa Mhe. Waziri wa Sheria. Lakini ninalotaka kumwambia kwamba sasa hivi karibu dunia nzima tayari wameanzisha vipindi au redio zile za Kiswahili zinazozungumzia Kiswahili. ukenda Marekani kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda China kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda Uingereza kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda Ufaransa kuna lugha ya Kiswahili, ukenda Ujerumani kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda Japan kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda Naigeria kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda Afrika ya Kusini kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda India kuna idhaa ya Kiswahili, ukenda Pakistani kuna idhaa ya Kiswahili na Misri hivyo hivyo na nchi nyengine. Kwa hivyo Kiswahili hiki sasa hivi kinakuzwa na sisi tukikuze tusibakie tu kuwa na makombo haya ya kikoloni. Ahsante, tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu 30 Lugha ya Mahakama
Kifungu 31 Ushahidi kwa Njia ya Video
Kifungu 32 Kunakili Ushahidi Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 33 Katazo la Vinasa Sauti na Kurikodi Video Kusikoruhusiwa
Kifungu 34 Muda wa kuweka kumbukumbu
Kifungu 35 Hukumu na Amri Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 36 Hkumu ya Mkato

SEHEMU YA SITA

Masharti ya Jumla

Kifungu 37 Naibu Mrajis Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 38 Uwezo wa Naibu Mrajis
Kifungu 39 Matokeo ya Kiapo Chenye Mapungufu
Kifungu 40 Uwezo wa Jaji Mkuu

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina pingamizi juu ya kifungu hichi hata kidogo lakini kuna neno ambalo nataka nipatiwe ufafanuzi.

Sheria nyengine husema kuwa pengine Waziri atatunga lakini kuna vifungu vyengine anaambiwa mtu yule anaweza kufanya suala lile, sasa mimi nataka nipate ufafanuzi kuhusu kuala hili anaweza na atafanya au atatunga. Kwa sababu juzi katika Mswada wa Mhe. Rashid Seif alikubali kuwa lazima Waziri atatunga.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kifungu cha 41 hicho.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: cha 41 au cha 40.

Mhe. Mwenyekiti: cha 41.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Aaah! Subiri Mhe. Mwenyekiti, Uwezo wa Jaji Mkuu kutunga Kanuni za Mahakama, hakijamaliza kwa sababu mwisho kuna kifungu cha 2(ii) au siyo.
Mhe. Mwenyekiti: Sawa.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Sasa kuna neno hapa Jaji Mkuu anaweza, sasa nataka nipatiwe ufafanuzi. Kuwa anaweza au atafanya au atatunga. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mjumbe. Wakati nikijumuisha hapa nilitoa ufafanuzi huo, nilisema katika utungaji wa sheria kuna mambo mawili, hapa tumesema kwamba Jaji Mkuu anaweza kutunga. Kwa hivyo hii tunasema inamruhusu Jaji Mkuu pale ambapo atahisi kwamba kuna haja ya kutunga kanuni, lakini ukisema kwamba Jaji Mkuu atatunga ina maana hiyo umemlazimisha kwa sheria kwa hivyo ni lazima atunge.

Sasa wakati mwengine inaweza ikawa hakuna haja ya kutunga hizo kanuni. Kwa hivyo kama hakuna haja tuseme tu, tumruhusu pale ambapo kuna haja ya kutunga kanuni basi ndio tukasema kwamba Jaji Mkuu anaweza kutunga kanuni. Lakini tukisema kwamba Jaji Mkuu atatunga kanuni basi lazima Jaji Mkuu atunge kwa sababu yule tumeshamlazimisha. Kwa hivyo tunapoandika kwamba anaweza ni nzuri zaidi kwa sabaub unampa uhuru pale ambapo pana haja ikitokea atatunga na pale ambapo hapana haja basi hawezi kutunga.

Lakini ukisema atatunga ina maana unamlazimisha hata kama hakuna haja madhani sheria imeshasema itabidi lazima atunge na itakuwa haina maana na ndio tofauti kubwa ya anaweza na atatunga.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi sitambui sheria lakini naona sheria nyingi zinapokuja lazima huwa kunautungaji wa kanuni. Sasa Mawaziri wengine wasitwambie kuwa Waziri anaweza kutunga Kanuni na sheria nyengine zikija tukaona kuwa waziri atatunga kanuni. Sasa pangelikuwa na suala moja ambalokuwa kila sheria inapokuja tuambiwe kuwa Waziri anaweza kutunga kanuni. Kama hakuweza itakuwa si lazima, lakini waziri mwengine akija na sheria tukiambiwa kwa kuwa huyu anaweza huyu tunaambiwa atafanya hivi, huwa mimi hili suala linanichanganya.

Mhe. Mwenyekiti, ndio nikaona nimuulize kuwa yeye ni mwanasheria kuwa kuna umuhimu wa ufanya hili au lazima aambiwe kuwa mtu anaweza. Ina maana siku nyengine atakuwa hawezi, pengine itakuwa anaumwa akasema mimi sikutunga kanuni kwa sababu naumwe. Sasa kama ni sheria inamlazimisha Waziri kurunga kanuni ambiwe kuwa Waziri atatunga kanuni au Mkuu yeyote yule ambayekuwa inamuhusu kutunga kanuni aambiwe kuwa atatunga kanuni .

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana mjumbe. Kwa kweli naomba ieleweke kwamba kuna baadhi ya sheria tunapozitunga kwa hivyo ni lazima uweke kifungu cha kusema kwamba Waziri atatunga sio anaweza. Kwa sababu ni lazima kwanza atunge zile kanuni ili ile sheria iweze kutekelezeka. Kwa mfano katika mambo mengi ya fedha kwa hivyo unatunga zile kanuni kwanza ili ziweze kutekelezekana ndani ya ile sheria.

Lakini kwa mfano sheria kama hizi pale haja kwa mfano inapotokea kwa mfano tunayo sheria hii lakini tukahisi kwamba kuna haja sasa ya kuzidisha kwa mfano ile Kamati kwa hivyo umeshasema kwamba waziri anaweza akatunga kanuni. Kwa hivyo pale ikiwa kuna haja hiyo ndio pale anaweza kutunga. Lakini sheria kama hii ukisema kwamba Waziri atatunga ina maana lazima ufanye kabla ya ile maana itakuwa haina maana. Kuna sheria nyengine ni lazima useme kwamba waziri anaweza kumpa nafasi pale inapotokea haja. Lakini kuna sheria nyengine lazima useme kwamba waziri atatunga yaani atunge zile kanuni zitumike pamoja na ile sheria. kwa hivyo kuyna sheria nyingi tu zitakuja nyengine kwamba waziri atatunga na nyengine waziri anaweza, kulingana na ile hali ya lile suala ambalo lipo katika mjadala.

Mhe. BikameYussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wanasheria kwa hivyo tuendelee.
Kifungu 40 Uwezo wa Jaji Mkuu Kutunga Kanuni za Mahakama Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 41 Uwezo wa Waziri Kuunda Kanuni

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar
(Divisheni ya Mahakama Kuu) ya Mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naomba Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Bishara Zanzibar Division ya Mahakama Kuu 2013 sasa usomwe kwa mara ya tatu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(*Muswada wa sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa***)**

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa ushirikiano mzuri mliotuonesha tangu kuanza Mswada huu wa Mahakama ya Biashara na hadi leo tumeupitisha. Sasa kabla sijaakhirisha nilikuwa nina tangazo moja muhimu niwatangazie waheshimiwa wote wa timu ya Baraza la Wawakilishi kwamba mazoezi yanaendelea katika uwanja wa Mau, kuanzia siku ya Alhamis, Ijumaa na Jumamosi. Cha msingi zaidi na muhimu kwamba tumeshiriki katika Sherehe za Mei Mosi na tumepangiwa kucheza na KMKM tarehe 14 mwezi wa 4. Kwa hivyo timu ya KMKM si t imu ndogo kwa hivyo tufanyeni mazoezi ili tuweze kuishinda timu hiyo ambayo ipo daraja la kwanza.

Baada ya tangazo hilo naomba niakhirishe kikao hichi hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 11/04/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:30 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 11/04/2013
Saa 3:00 asubuhi)